

UZINDUZI WA VITABU VYA MAELEKEZO YA JINSI YA KUBORESHA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI WILAYA YA UKEREWE.

UTANGULIZI

Vitabu viwili vilivozinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndugu Kassim Majaliwa Kassimu Kitaifa, vinaelezea changamoto zilizopo katika kuinua ufaulu kwa Shule za Awali na Msingi hata hivyo, vitabu vinaelezea jinsi ya kukabiriana na changamoto hizo.

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kuitia Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule, Maafisa Elimu Kata, Maafisa kutoka Halmashauri pamoja na Viongozi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Viongozi wa Kisasa, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii wakiongozwa na Mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya kwa pamoja walikutana kwa ajili ya kufanya uzinduzi huo katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Bukongo tarehe 08/09/2022.



Mwakilishi wa Mkuu wa wilaya Zebeda Kimario akifungua Mwonozo wa mafunzo tarehe 8.09.2022

Aidha, Viongozi wote walisisitiza suala ya kufuata maelekezo na miongozo wakati wote wa kutekeleza majukumu ya kazi. Waliipongeza Serikali kwa kutoa hiyo miongozo kwani itasaidia Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kutembea kwa pamoja na kuhakikisha inapata matokeo ambayo ndio hasa wananchi wanategemea kuyaona.

Hata hivyo, washiriki waliaswa kuhakikisha wanabuni mbinu nyingi katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kufuata miongozo iliyotolewa ili kuhakikisha suala la Elimu linaboreshw na Ukerewe ipate kuonekana katika ufaulu uliobora.

UZINDUZI

Mgeni Rasmi aliwaambia washiriki wa uzinduzi kuwa, elimu itaboreshw pale tu ambapo walimu kama kioo cha jamii watatoa elimu kwa jamii kuhusu kukomeshwa kwa utoro mashuleni na kukomesha kabisa suala la mimba mashuleni ili watoto waweze kufikia malengo yao. Aidha Mgeni Rasmi alizindua vitabu vya maelekezo ambavyo ni “Changamoto katika Uboreshaji Elimu Msingi na Sekondari na nini kifanyike?” na kitabu cha Mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya Elimu Msingi” kwa kuwapa hivyo vitabu Maafisa Elimu Kata 25 kama ifuatavyo

1. Afisa Elimu Kata, Kata ya Bukongo
2. Afisa Elimu Kata, Kata ya Ngoma
3. Afisa Elimu Kata, Kata ya Bukiko
4. Afisa Elimu Kata, Kata ya Bwisya
5. Afisa Elimu Kata, Kata ya Muriti
6. Afisa Elimu Kata, Kata ya Nyamanga
7. Afisa Elimu Kata, Kata ya Bukungu
8. Afisa Elimu Kata, Kata ya Irugwa
9. Afisa Elimu Kata, Kata ya Ilangala
10. Afisa Elimu Kata, Kata ya Kakukuru
11. Afisa Elimu Kata, Kata ya Namilembe
12. Afisa Elimu Kata, Kata ya Nduruma
13. Afisa Elimu Kata, Kata ya Bwiro
14. Afisa Elimu Kata, Kata ya Igalla
15. Afisa Elimu Kata, Kata ya Mukituntu
16. Afisa Elimu Kata, Kata ya Murutunguru
17. Afisa Elimu Kata, Kata ya Kagunguli
18. Afisa Elimu Kata, Kata ya Namagondo
19. Afisa Elimu Kata, Kata ya Bukindo
20. Afisa Elimu Kata, Kata ya Kagera
21. Afisa Elimu Kata, Kata ya Bukanda
22. Afisa Elimu Kata, Kata ya Kakerege

23. Afisa Elimu Kata, Kata ya Nakatunguru
24. Afisa Elimu Kata, Kata ya Nkilizya
25. Afisa Elimu Kata, Kata ya Nansio

MADA

CHANGAMOTO CHANGAMOTO KATIKA UBORESHAJI ELIMU MSINGI NA SEKONDARI NA NINI KIFANYIKE?"



Katika kuwasilisha mada kwa washiriki wa uzinduzi wa vitabu vya miongozo, wawasilishajis walibainisha changamoto mbalimbali zinanzozikabiri sekta ya elimu ya msingi na sekondari katika utekelezaji wake. Changamot hizo ni pamoja na:-

1. Kuongezeka kwa wanafunzi wanaoandikishwa kuanza darasa la awali na darasa la kwanza
2. Kuongezeka kwa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba bila kufaulu ili kuendelea na masomo
3. Uwepo wa wanafunzi wanaofaulu kidato cha nne na kukosa nafasi za kuendelea na masomo ya sekondari
4. Uwepo wa wanafunzi wanaokosa umahili wa lugha ya kiingereza
5. Uwepo wa wanafunzi wanaoshindwa kumaliza shule
6. Upungufu wa walimu
7. Udhifu wa baadhi ya viongozi katika usimamizi na ufuatiliaji na
8. Walimu kukosa molari ya kufanya kwa kukosa motisha



Aidha, AFISA ELIMU SEKONDALI alibainisha namna bora ya kukabiriana na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo

- Uandikishaji wa wanafunzi uanze mwezi Oktoba hadi mwezi Desemba
- Walimu wabuni mbinu bora ya ufundishaji na ujifunzaji
- Kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika alama za ufaulu wa A na B kwa kuongeza juhudni na maarifa katika ufundishaji na ujifunzaji
- Kuwepo kwa ratiba ya walimu kujengeana uwezo mahala pakazi
- Nafasi za wanafunzi kuijunga a kidato cha tano ziongezwe ili wanafunzi wote waliofaulu kidato cha nne wapate nafasiz za kuendelea na masomo
- Kuandaa mkakati kabambe wa kutoa huduma ya chakula mashulenii
- Mafunzo wa ualimu vyuoni uongezewewe muda wa mwaka mmoja ili kuwaimarisha vizuri walimu
- Walimu walioonyesha bidii katika kazi zao wapewe motisha

HALI YA UTOAJI WA ELIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Katika hii mada, mwezeshaji alibainisha changamoto ambazo zipo katika hali ya utoaji wa elimu katika Shule za Msingi na Sekondari kama ifuatavyo:-

- Baadhi ya wanafunzi kutomudu stadi za KKK
- Upungufu wa Walimu
- Utoro wa wanafunzi

HATUA

- Ili kuondosha changamoto ya utoro, Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na 1965 na Kanuni zake za Elimu za mwaka 2002, atakayesababisha utoro wa mwanafunzi atakabiriwa na kosa hilo ambapo atatakiwa kutoa faini ya Tshs. 30,000/- na isyozidi Tshs. 50,000/- au kufungwa jela mizi sita (6) au vote kwa pamoja. Hivyo basi, washiriki walisisitizwa kutumia hiyo sharia ili kukomesha utoro mashulen.
- Kumwezesha mwanafunzi kujua teknolojia ya habari
- Kumwezesha mwanfunzi kujiaamini
- Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa
- Kuhakikisha wanafunzi darasa la pili wanamudu stadi za KKK
- Kuongeza wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi

Katika mjadala wa mada zote, washiriki waliiomba Serikali kuhakikisha inaongeza walimu ili kukabiliana na namba kubwa ya wanafunzi mashulen aidha, waliiambaia meza kuu kuwa suala la kuanzishwa kwa chakula mashulen lina changamoto kwani wazazi kuchangia chakula ni vigumu na hata hivyo shule ambazo zinalima chakula kwenye mashamba ya mashule, kile chakula kinavurugwa na mifugo na hata hivyo rutuma imeshuka hivyo wakaomba Idara ya Kilimo na Mifugo iwasaidie katika hilo.

Katika majibu, washiriki walielezwa kuwa, shule ambazo zina uhitaji wa Maafisa kilimo wawasiliane na Maafisa Kilimo hao kwani wanapatika kwenye Kata aidha, mifugo ambayo inaharibu mazao, maafisa watendaji watunge sharia ndogo zitakazowabana wafugaji ili waweze kufunga mifugo yao. Katika suala la jamii kutochangia chakula mashule, washiriki walielezwa kuwa, wahakikishe suala la chakula linakuwa agenda ya WDC ili suala hilo literemke kwa Watendaji wa Vijiji na jamii iapate elimu ya kutosha ili waweze kuchangia chakula kitu ambacho kitapandisha ufaulu wa wanafunzi.

Mgeni rasmi aliwashukuru washiriki wa uzinduzi huo na kuwataka kwenda kutekeleza yale yote yaliyosisitizwa kwenye kikao hicho aidha, aliwataka kuhakikisha wanakuwa na mbinu mbadala ili kuhakikisha wanapata matokeo yaliyo mazuri bila kuathiri maelekezo na miongozo ya Elimu